UWAZI WA MANUNUZI YA UMMA

Open (Public) Contracting PAC Training, Dodoma

Dr. George Nsorani, October 2018
M&E Manager

Hivos people unlimited

Connecting Governments, Civil Society and Business to Open Up and Monitor Public Contracting

Tanzania Media Foundation

MSINGI WA KIKATIBA

WAJIBU WA SERIKALI, BUNGE NA MAHAKAMA KWA UMMA NA USHIRIKI WA UMMA KATIKA SHUGHULI ZA SERIKALI

Umma huweza kushirikiana na serikali kupitia vyombo vya habari rasmi, huru na vyenye ueledi kwa kupata **taarifa muhimu** na za kweli kuhusu shughuli za serikali yake

Umma huiweka madarakani serikali uipendayo na kuiamini ili kutawala kwa niaba yake na kwa **ustawi wake**.
(Ibara ya 8 ya katiba)

Umma hulichagua bunge ili kuwa mwangalizi, mlinzi na **msimamizi** wa serikali kwa **ustawi na maslahi** yake. Bunge huwajibika moja kwa moja kwa wananchi
(Ibara ya 63 (2))



Wajibu mkuu wa serikali - **ustawi wa wananchi**
(Ibara ya 8)
Serikali inawajibika kwa umma katika kuhakikisha kwamba ibara ya 9 ya katiba inatekelezwa.

Waajibu mkuu wa umma ni kushiriki katika shughuli za serikali kwa mujibu wa ibara ya 8 na 27, 28 za katiba.. Ili kutekeleza wajibu wake serikali huwa na wajibu wa kuushirikisha umma

Serikali na umma hutekeleza wajibu wao kwa mujibu wa katiba na sheria chini ya mahakama huru

Kamanzi D.R, 2018

MCHAKATO MZIMA WA MANUNUZI YA UMMA

TULIPOTOKA, TULIPO NA TUNAKOTAMANI KUWA

HAPO AWALI:
Usiri katika mchakato mzima wa mikataba

SASA:
Uwazi wa mikataba

TUNAKOTAMANI:
Uwazi katika mchakato mzima wa mikataba



MIPANGO

Bajeti, Mipango ya mradi, mipango ya manunuzi, tafiti za masoko na taarifa kwa umma.

UANZISHAJI/ZABUNI

Taarifa ya zabuni, mahitaji mahususi
Kuangalia thamani
Kutagaza zabuni

UTOAJI MKT

Maelezo ya mikataba, Taarifa za mzabuni, Tathmini ya zabuni, thamani (maadili)

MIKATABA

Maelezo ya mwisho, mkataba uliosainiwa, marekebisho ya mkataba, maadili.

UTEKELEZAJI

Taarifa za maendeleo ya utakelezaji, mahali, kuongezeka muda, marekebisho, taarifa za umaliziaji au ustishwaji.

UWAZI WA MIKATABA

Uwazi wa mikataba ni uwekaji na upatikanaji rahisi wa mikataba inayohusu rasili-mali za umma iliyoingiwa kati ya Serikali na makampuni

UWAZI WA MANUNUZI YA UMMA

Huu ni uwazi ambao uhusisha umma katika mchakato wote wa utayarishaji zabuni mpaka utekelezaji wake. Ni mchakato wa wazi, wa haki, na wenye ufanisi: tokea hatua za upangaji, utoaji wa zabuni, ugawaji linganifu (Utoaji tuzo) na utoaji wa mikataba hadi utekelezaji

UWAZI WA MANUNUZI YA UMMA NI NINI?



Uwazi wa manunuzi ya umma inahusu kuchapisha na kutumia habari wazi, kupatikana kwa wakati taarifa juu ya mchakato wa mikataba ya serikali ili **kushirikisha** wananchi katika kutambua na kutatua kero zinazowakumba.



VIPENGELE MUHIMU

Uwepo wa data wazi kwa umma juu ya mipango, manunuzi, na usimamizi wa mikataba ya umma.

Huu ni shiriki na matumizi ya data za mikataba unaofanywa na watendaji wasio wa serikali katika kupanga, kutoa, na kufuatilia mikataba.

Uwajibikaji na urekebishaji ufanywao na mashirika ya serikali au makandarasi kwa kufanyia kazi maoni wanayopokea kutoka kwa umma, mashirika ya kiraia na makampuni, na kuleta ufumbuzi.

Manunuzi na uingiaji wa mikataba ya umma huboreka

ATHARI ZA KUTOKUWEPO UWAZI NA USHIRIKISHWAJI WA UMMA

Kutoweza kuona mikataba kunazuia wananchi wasiweze:-

Kupata taarifa sahihi, kunapunguza hali ya kujiona kuwa ni wamiliki wa rasilimali zao na kunapunguza ari na uwezo wao wa kusoma kwa uangalifu na kushiriki kikamilifu katika majadiliano au maamuzi kuhusu jinsi nchi inavyopaswa kusimamia rasilimali zake.

KANUNI ZA KIMATAIFA ZA UWAZI WA MANUNUZI YA UMMA



1. Haki ya kupata taarifa kuhusiana na mikataba ya manunuzi ya umma
2. Uwazi na usawa
3. Uchapishwaji wa habari za mikataba kwa wakati.
4. Kukusanya, kusimamia, kurahisisha na kuchapisha taarifa/takwimu za mikataba
5. Kutambua haki ya umma kushiriki katika usimamizi na kuwekewa mazingira wezeshi kwa ushauri na uangalizi wa umma.
6. Serikali kwa ushirikiano, kujenga uwezo wa wadau ili kuelewa,kufuatilia na kuboresha mikataba ya umma.
7. Serikali kuunda mifumo endelevu ya kifedha ili kusaidia ushirikishwaji wa umma katika mchakato mzima wa manunuzi ya umma.
8. Kuhimiza mazungumzo/midahalo na kufanyia kazi maoni ya umma

FAIDA ZA KUWEPO UWAZI WA MANUNUZI YA UMMA

- Uwazi wa manunuzi ya umma ni mahali ambapo manufaa ya umma hupatikana; pesa za walipa kodi hugeuzwa kuwa shule, barabara, hospitali, hugeuzwa katika vitu ambavyo ni muhimu kwa watu wa kawaida.

- Kila mwaka, Serikali hutumia kiasi kikubwa cha fedha kupitia mikataba, katika kila kitu kutoka penseli na karatasi mpaka kwenye ujenzi wa miradi mikubwa ya miundombinu kama vile viwanja vya ndege.

- Uwazi wa manunuzi ya umma hutoa makubaliano bora kwa serikali, huziwezesha sekta binafsi kushiriki, na kuwezesha kuwepo kwa bidhaa na huduma bora.

Fedha huongezeka thamani

Mazingira ya biashara huwa ya haki zaidi



Utekelezaji bora zaidi

Wizi na rushwa hupungua

Thank You!

Hivos
people unlimited

Connecting Governments, Civil Society and Business to Open Up and Monitor Public Contracting